

**P1 – Y2 – KISWAHILI - LUGHA
MTIHANI WA MWIGO – PP1
MACHI, 2019**

MUDA: SAA 2½

KWA MATUMIZI YA MTIHANI

SEHEMU	SWALI	UPEO	TUZO
A	1	20	
B	2	20	
C	3	50	
D	4	10	
	JUMLA	100%	

SEHEMU YA ‘A’ - INSHA (Alama 20)

1. Andika insha isiyopungua kurasa mbili kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo.
 - a) Kumekuwa na ongezeko la migomo ya wafanyakazi nchini katika siku za hivi karibuni. Wewe ni katibu wa tume iliyobuniwa na Rais kusimamia suala hili. Andika ripoti.
 - b) Ufisadi umechangia pakubwa kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Jadili.
 - c) Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: “Ulimi huuma kuliko meno.
 - d) Lo, yaliyotendeka katika makazi ya Jirani yetu usiku huo yalikuwa ya kutisha sana. Kumbe watu wamegeuka hayawani! Hayawani!.....

SEHEMU YA ‘B’ - UFAHAMU (Alama 20)

UFAHAMU.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

Vitabu vingi vya hadithi za watoto vilivyowahi kuandikwa katika lugha ya Kiswahili kufikia sasa vinaweza tu kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa darasa la nne hadi la nane na hivyo basi kuacha ombwe pale panapostahili kuwekewa msingi imara - shule ya chekechea hadi darasa la tatu. utafiti uliowahi kufanywa na wanaisimu-saikolojia unathibitisha kwamba uwezo wa mwanafunzi wa kujifunza lugha ya pili huwa katika kiwango cha juu awapo na umri mdogo na kwamba uwezo huo huanza kupungua kadiri umri unavyoongezeka na kufikia kipindi maalum (critical period) ambacho hukisiwa kubisha katika umri wa kubaleghe au kuvunja ungo.

Hivyo basi, ili kustawisha hulka ya usomaji ya kudumu, waandishi wa fasihi ya watoto wanapaswa kujifahamisha mengi kuhusu ukuaji wa watoto hao wadogo na mikakati ambayo huitumia katika kujifunza lugha ya pili.

Aidha, wanapaswa kuyafahamu yale yanayowapendeza na kuwachochea katika kusoma ili kuyajumuisha katika vitabu vyao vya hadithi. Mambo haya yatatimia iwapo waandishi hao watakuwa na mafunzo ya kimsingi katika taaluma ya isimusaikolojia.

Wanafunzi katika viwango tofauti wana mikakati tofauti ya kujifunza lugha ya Kiswahili. Kufikiria kwamba wanafunzi wa madarasa ya chini (darasa la kwanza, pili na tatu) wanaweza kuitumia mikakati sawa na ile ambayo hutumiwa na wenzao wa madarasa ya juu kujifunza Kiswahili si sahihi.

Watoto wadogo hujifunza mambo mengi kwa kukariri, kuigiza, kuiga, kufuatilia hadithi kwa picha miongoni mwa mbinu nyingine. Ili kufanikiwa katika kuwaandikia, sharti mikakati hiyo ya ujifunzaji izingatiwe.

Ufundi mkubwa unahitajika si tu katika kuziunda sentensi zao bali pia katika kuifinyanga sarufi. Sentensi zenyewe ziwe fupi, zenye sarufi na msamiati sahili, zilizorudiwarudiwa ili kuzifanya zinate akilini na kuendelezwa kwa mtindo wa nyombo au mashairi mepesi.

Watoto wadogo huvutiwa sana na nyimbo na mashairi mepesi na hujifunza kwa urahisi kupitia kwayo. Msururu wa vitabu vya ‘Someni kwa Furaha’ uliotumiwa katika miaka ya themanini na mwanzomwanzo wa miaka ya tisini ni mfano wa vitabu vilivyotekeleza dhima muhimu sana katika kuumua na kuchochea hamu ya wanafunzi kupenda kukisoma Kiswahili.

Vitabu hivyo vilitumia mbinu mbalimbali zilizoweza kuyateka mawazo ya wanafunzi katika viwango tofauti. Miongoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya vibonzo, mashairi na nyimbo za chekechea zenye maudhui ambayo watoto wangeweza kujinasibisha nayo. Baadhi ya nyimbo hizo zilihimiza umuhimu wa kusomea katika mazingira safi, ushirikiano katika shughuli mbalimbali na umuhimu wa kuyachangamkia masomo. Mfano mzuri ni huu wimbo unaopatikana katika kimojawapo cha vitabu katika msururu huo: *Chawa chawa mchafu, petu ni pakavu Kata nyika utosini, kata nywele kwa mashine Kichwa safi kama nini? Chawa chawa mchafu, petu ni pakavu.*

Mbinu nyingine iliyotumiwa sana katika vitabu hivyo ni matumizi ya picha na vibonzo. Vitabu vya watoto vinapaswa kuwa na picha nyingi au vibonzo vingi kuliko maandishi. Picha na vibonzo vyenyewe viwe vya rangi kwa sababu watoto huvutiwa sana na rangi.

Waandishi wa fasihi ya watoto katika Kiingereza wamefanikiwa pakubwa katika kukumbatia mbinu hii na hivyo basi kuyakidhi mahitaji ya rika tulilolitaja kwa kuandika vitabu ambavyo vimechangia kwa akali kubwa katika kustawisha hulka ya usomaji kuanzia shule ya chekechea hadi darasa la nane. Hali hii ni tofauti na Kiswahili ambapo hulka ya usomaji bado ingali changamoto kubwa kwani huanza kuwekewa msingi katika darasa la nne.

Kiini hasa cha kuendelea kuwepo kwa mielekeo hasi na matokeo mabaya katika somo la Kiswahili ni kule kukosekana kwa vitabu faafu vya hadithi za watoto katika madarasa ya chini vinavyoweza kusaidia katika kujenga hulka ya usomaji mapema iwezekanavyo.

Ombwe hilo linaweza kufidiwa tu iwapo waandishi wataibuka na vitabu ambavyo vitayakidhi mahitaji ya watoto hao wadogo na kuwapa ari ya kukipenda Kiswahili kuanzia umri wa chini.

Maswali.

1. Kipe kifungu anwani mwafaka na utoe sababu **Ala.2**
2. Ni katika umri gani mwanafunzi hujifunza lugha ya pili kwa urahisi? **Ala.1**
3. Waandishi wa vitabu vya watoto watastawisha usomaji wa kudumu kwa njia gani? **Ala.4**
4. Taja dhana potovu kuhusiana na ujifunzaji lugha kwa watoto. **Ala.2**
5. Onyesha njia ambazo kwazo watoto hujifunza kwa wepesi. **Ala.4**
6. Vitabu vya watoto vinapendekezwa viwe na sifa gani? **Ala.3**
7. Eleza maana ya msamiati huu kulingana na muktadha wa matumizi. **Ala.4**
 - (a) kubaleghe.
 - (b) Ombwe.
 - (c) Kufidiwa.
 - (d) Isimusaikolojia

SEHEMU YA ‘C’ - MATUMIZI YA LUGHA (Alama 50)

- a) Onyesha silabi inayowekewa shadda kwenye maneno haya. **Ala.2**
 - i. Karatasi _____
 - ii. Samahani _____

- b) Andika sentensi hizi kwa udogo. **Ala.2**
- i. Sijui kwa nini hindi lake ni bichi.
- ii. Mlete huyo mwizi afunguliwe mashtaka.
- c) Eleza matumizi ya KWA katika sentensi zifuatazo. **Ala.2**
- i. Wanawake kwa wanaume walifika mkutanoni.
- ii. Yule mtaalam alieleza maana ya utandawazi kwa ufasaha.
- d) Onyesha aina ya vitenzi katika sentensi. **Ala.2**
Wewe umewahi kufika shule ukiwa umechelewa?
- e) Onyesha aina za virai kaika sentensi. **Ala.2**
Gari lao lilianguka kando ya jengo.
- f) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo. **Ala.2**
- i. Chakula chote kitaharibika.
- ii. Chakula chochote kitaharibika.
- g) Eleza matumizi ya vile katika sentensi hii. **Ala.1**
Vile vile seremala alitengeneza meza.
- h) Tunga sentensi ukitumia kivumishi cha pekee ‘o-ote’ katika ngeli ya U – U. **Ala.1**
- i) Neno ‘huyu’ limetumikaje (kumaanisha nini katika sentensi hizi). **Ala.2**
- (i) Huyu amekuja kwangu.
- (ii) Mgeni huyu amekuja kwangu.
- j) Tunga sentensi ukitumia kielezi cha:- **Ala.2**
- i. Namna/jinsi.
-
- ii. Idadi.
-
- k) Kanusha sentensi ifuatayo. **Ala.1**
Mlevi alitembea kiholela halafu kaanguka chini pa!
-
- l) Akifisha sentensi ifuatayo. **Ala.2**
nilimkuta mkuu wa wilaya ya fahari akisoma kitabu kiitwacho utubora mkulima
-
- m) Sahihisha sentensi ifuatayo kwa njia tatu tofauti. **Ala.3**
Hapo ndimo alikofia.
-
- n) Andika katika usemi wa taarifa. **Ala.2**
“Hivi vibanda vinatumia kulanguzia dawa za kulevya”, Mku wa polisi alilalamika.
-
- o) Tumia Mchoro wa matawi kuichanganua sentensi ifuatayo. **Ala.3**
Mwanafunzi mzuri ametunukiwa zawadi.
- p) Tofautisha kati ya: /e/ na /u/. **Ala.2**
-
- q) Eleza matumizi ya alama zifuatazo za uakifishi. **Ala.2**
- i. Alama za mdokezo/dukuduku.
-
- ii. Kistari kirefu.
-
- r) Andika katika wingi karibu. **Ala.2**
Mtu yuyo huyo aliubeba mzigo uo huo licha ya kukanywa.
-
- s) Andika kwa wastani. **Ala.1**
Magoma haya yatachezwa wanjani.
-
- t)

- i. Mahali palipohamwa panaitwa? **Ala.1**
-
- ii. Ugonjwa wa kuvimba jicho huitwa vipi? **Ala.1**
-
- iii. Nini maana ya 'kidani'. **Ala.1**
-
- iv. Andika tarakimu hii kwa maneno: 110,010. **Ala.1**
-
- v. Huyu ni mnyama yupi "mbega". **Ala.1**
-
- u) Andika maana ya nahau hizi. **Ala.2**
- i. Vaa miwani.
-
- ii. Kula yamini.
-
- v) Mshipi hufungwa kiunoni, pia _____ na _____ hufungwa kiunoni. **Ala.2**
- w) Taja rangi ya kwanza na ya mwisho katika upinde wa mvua. **Ala.2**
-
- x) Ziandike sentensi zifuatazo kwa kutumia kirejeshi amba- **Ala.2**
- i. Mayai yaliyokaangwa yameliwa.
-
- ii. Ukweli uliobainika umetusaidia.
-
- y) Anza sentensi zifuatazo kwa kutumia neno lililowekwa kwenye mabanu. **Ala.2**
- i. Nyimbo alizoimba zilifanya akachaguliwa. (*kuimba*)
-
- ii. Alibisha mara nyingi ndipo akafunguliwa. (*kubisha*)
-

SEHEMU YA 'D' - ISIMU JAMII (Alama 10)

1. Eleza njia za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. **Ala.4**
-
- 2.
- a) Fafanua mtindo wa lugha uliotumiwa katika taarifa ifuatayo huku ukieleza sababu za matumizi ya vitambulisho maalum vya lugha. **Ala.3**
- Wananchi, mimi sina mengi. Hapana katika nyinyi asiyenielewa. Sina la kusema, ila ninawakumbusheni kuwa mnahitaji kiongozi atakayeshughulikia maslahi ya taifa zima. Mtu huyo ni mimi na ninajitahidi niwezavyo kujenga masoko, barabar, shule. Zaidi na mazahanati na maisha yenu yatakuwa ya raha zaidi.
-
- b) Thibitisha kuwa adabu za lugha hazizingatiwi miongoni mwa wanajamii siku hizi. **Ala.3**
-